JINSI CHANJO ZA COVID-19 ZINAFANYA KAZI

120221 KISWAHILI

Chanjo za COVID-19 zinakukinga dhidi ya ugonjwa

Wataalamu wa afya wa ngazi ya chini, mkoa, na kitaifa wanapendekeza kupata chanjo dhidi ya COVID-19. Kwa sasa, kuna chanjo 3 zilizoidhinishwa nchini Marekani — Pfizer/BioNTech, Moderna na Johnson & Johnson.

Ni kawaida kupata chanjo zaidi ya moja ili kupambana na virusi hivyo hivyo. Kila moja ya chanjo hizi zimethibitishwa kuwa salama na madhubuti katika kuzuia homa kali au kifo kitokanacho na COVID-19.

Wataalamu wa tiba bado wanajifunza ni muda gani chanjo hizi zinakukinga na ikiwa zitakuzuia kueneza COVID-19. Inaweza kuchukua muda fulani kabla ya watu wengi zaidi kupatiwa chanjo ambayo kwayo tunaweza kuacha kutumia kinga za kila siku. **Endelea kunawa mikono, kuvaa barakoa, kudumisha umbali, na kupunguza ukubwa na muda wa mikusanyiko, hata kama umepata chanjo.**

Zinachofanya

- **Zinaufundisha mwili wako jinsi ya kutambua na kupambana na virusi vya korona ambavyo husababisha COVID-19.**
- Chanjo za Pfizer na Moderna zina messenger RNA (mRNA). mRNA ni kama mwongozo. Inaufundisha mwili wako jinsi ya kutengeneza protini isiyo na madhara ambayo inaonekana kama protini iliyo kwenye virusi hivi vya korona. Mwili wako huikubali protini na kuunda chembe hai zinazopambana na magonjwa na kingamwili ambazo zinaweza kutambua na kupambana na virusi hivi vya korona.
- Chanjo ya Johnson & Johnson ni chanjo ya virusi vya vector. Ina virusi salama vya adeno, kutoka kwenye familia ya virusi ambavyo vinasababisha mafua ya kawaida. Virusi vya adeno vilivyo katika chanjo vinabeba jeni kutoka kwenye protini ya mwiba ya virusi vya korona. Hii inaufundisha mwili wako jinsi ya kutambua na kupambana na virusi vya korona ambavyo husababisha COVID-19.
- **Aina yoyote ya chanjo utakayopatiwa, mwili wako utakuwa tayari kukulinda iwapo itaona virusi vya korona hapo baadaye.**

Kile aambacho hazifanyi

- **Hazina** virusi vya korona na **haziwezi kukuambukiza** COVID-19.
- **Hazibadilishi**DNA yako au vinasaba vyako.
- **Hazisababishi**utasa.

Je, chanjo za COVID-19 zina nini hasa?

Chanjo ya Pfizer na Moderna zina mRNA na viambata ili kuisaidia mRNA kufanya kazi mwilini mwako: mafuta, potasiamu, misombo ya kaboni ili kulinda mRNA kutokana na asidi, chumvi, na sukari nyingi.

Chanjo za Johnson & Johnson zina virusi vya adeno vilivyoboreshwa kwa taarifa kutoka kwenye virusi vya korona. Pia zina viungo vinavyosaidia kuifanya kuwa imara: chumvi, sukari na michanganyo mingine ya kaboni.

Chanjo hizi **hazina** mayai, vihifadhi, lateksi, nyama ya nguruwe au bidhaa nyingine za wanyama, au chembe hai za kijusi.

Je, nani anaweza kupata chanjo hizi?

Wakazi wote wa Oregon wenye umri wa miaka 5 na zaidi wanastahiki kupata chanjo ya COVID-19. Watu wenye umri wa miaka 5-17 lazima wapate chanjo ya Pfizer. Watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kupata yoyote kati ya chanjo zinazopatikana.

- Ni mjamzito au unanyonyesha, au
- Una mzio wowote mbaya

Wanasayansi wanashughulikia chanjo kwa ajili ya watoto na vijana wenye umri chini ya miaka 5.

Madhara

Watu wengi hupata athari ndogo baada ya kupata chanjo. Hii ni ishara kwamba mwili wako unafanya kile kinachopaswa kufanywa: kujenga kinga dhidi ya ugonjwa.

- Madhara yanayotokea sana ni pamoja na uchungu au wekundu mahali ulipodungwa sindano ya chanjo, maumivu ya kichwa, uchovu, na/au homa ndogo (chini ya 100.4). Dalili hizi zinatokea sana baada ya dozi ya pili.
- Dalili hizi mara nyingi huondoka zenyewe baada ya siku chache. Yasipoondoka, mpigie simu daktari au kliniki yako.

Matatizo adimu, lakini makubwa

Ni adimu, lakini baadhi ya watu huwa na athari mbaya ya mzio kutokana na chanjo. Watu hawa wote walipata msaada wa kitabibu mara moja.

- Kila mtu anayepata chanjo hizi lazima asubiri angalau dakika 15 baadaye, ili wahudumu wa afya waweze kuwasaidia ikiwa watapata athari.
- Ikiwa umepata athari mbaya za mzio hapo awali, zungumza na daktari au kliniki yako.

Chanjo ya Johnson & Johnson inaweza kuhusishwa na tatizo adimu, lakini kubwa la kuganda damu. Baada ya utafiti wa kina, wafanyakazi wa afya wa taifa na jimbo wamekubaliana kwamba chanjo ya Johnson & Johnson ni salama kutumiwa.

Iwapo umepatiwa chanjo ya Johnson & Johnson, jifuatilie mwenyewe kubaini dalili hizi kwa wiki tatu baada ya kudungwa sindano:

- maumivu makali ya kichwa au maumivu ya kichwa yasiyoisha
- kutoweza kuona vizuri
- maumivu ya kifua au maumivu makali ya tumbo
- kuvimba au maumivu ya miguu
- kupumua kwa shida
- kuchubuka kwa urahisi au madoa madogo ya damu kwenye ngozi yako nje ya sehemu uliyodungwa sindano

Iwapo una dalili yoyote kati ya hizi, piga simu 911 au tafuta msaada wa matibabu. Ni muhimu kuwafahamisha kwamba ulipatiwa chanjo ya Johnson & Johnson hivyo wataweza kukuhudumia kwa njia ifaayo.

Msaada unapatikana ikiwa una maswali au wasiwasi

Unaweza kuhisi kuwa na matumaini kwamba chanjo zinaweza kutufanya tuwe karibu na wale tuwapendao tena. Unaweza kuhisi wasiwasi. Ikiwa wewe ni mtu wa rangi, unaweza kujiuliza ikiwa unaweza kuamini chanjo kutoka kwenye mfumo wa matibabu ambao umepoteza imani katika jamii yako hapo awali. Ubaguzi wa kimatibabu hapo awali na sasa unadhihirika wazi. Inaeleweka kuwa na wasiwasi. **Pata maelezo zaidi na upate usaidizi**:

- Zungumza na daktari au kliniki yako. Ikiwa huna daktari, piga simu 211 kwa pupiga simu 2-1-1 au 1-866-698-6155.
- Piga simu kwa Laini ya Usaidizi wa Usawa wa Ukabila wa Jimbo Zima la Oregon ikiwa umeathiriwa kiakili na kihisia na ubaguzi wa rangi: 503-575-3764 | linesforlife.org/racial-equity-support-line
- Piga simu ya Msaada Salama + Thabiti ya Jimbo Zima la Oregon kwa ajili ya msaada wa kihisia na kielekezi cha nyenzo. Si lazima uwe katika shida. 1-800-923-HELP (4357) | linesforlife.org/obhsl/

Tafuta "COVID-19" kwenye tovuti ya county yako ili kupata taarifa ya mahali husika.

Clackamas County

Columbia County Oregon

Multnomah County Health Department

Washington County Oregon